*Toleo 56 - Muharram 1443 AH / Septemba 2021 M*

# UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Hizb ut-Tahrir Kenya yafaulu kutamatisha kampeni yake ya Kiuchumi

**HABARI NA MAONI**
AU kama Mtangulizi wake OAU ni Zana ya Kikoloni

**TOLEO**
Uchumi Muovu Wa Kibepari Ndio Chanzo Cha Msoto

**JIBU LA SWALI**
Athari za Kisiasa nchini Afghanistan



KUMB: 01/1443 Jumatano, 03 Muharram 1443 H 11/08/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Hizb ut-Tahrir Kenya yafaulu kutamatisha kampeni yake ya Kiuchumi chini ya kauli mbiu- Msoto wa Kiuchumi Uislamu ndio Jibu.

Kwa rehema za MwenyeziMungu SWT, Harakati ya Hizb ut-Tahrir Kenya imetamatisha kampeni yake ya kiuchumi ilioanza tarehe 11 Julai 2021,na kutamatika tarehe 11 Agosti 2021.

Kampeni hii ilihusisha msururu wa amali; Darasa kubwa misikitini, ziara za mitaani na mazungumzo ya mitandaoni. Na katika Ijumaa ya mwisho ya mwezi mtukufu wa Dhulhijja Hizb ut-Tahrir Kenya ikagawanya toleo lililobeba anwani: **‘Mfumo muovu wa Kiuchumi wa Kibepari ndio chanzo cha Msoto wa Kiuchumi Ulimwenguni’**. Toleo hilo liligawanywa katika Miji ya Nairobi na ile ya pwani ikiwemo Mombasa, Kilifi, Malindi na Kwale.

Katika kipindi chote cha kampeni, Hizb ut-Tahrir/Kenya iliweza kufafanua kwa uwazi uhalisia wa mfumo muovu na potofu wa Uchumi wa Kibepari na namna ulizalisha msoto wa kiuchumi kwa umma. Kwa upande mwengine, Hizb pia ikaweka sura wazi kwa umma ya mfumo wa Kiuchumi wa Kiislamu uliotekelezwa kwa karne 13 na serikali ya Kiislamu ya Khilafah na kivitendo ukasuluhisha matatizo ya kiuchumi, sambamba na kuonyesha pia jinsi serikali hiyo ya Khilafah itakayosimamishwa hivi karibuni itakavyotatua matatizo ya kiuchumi.

Hashtegi za kampeni hii zilikuwa:

**Kiswahili: #Msotowa_Kiuchumi_Uislamundio_Jibu**
**English: # EconomicHardships_IslamIsTheSolution**

Tunamuomba MwenyeziMungu SWT atupe Khilafah chini ya mfumo wa Utume ambayo kwa hakika itakomboa walimwengu kutokana na umasikini uliozaa. Na mwisho wa dua zetu ni kwa sifa njema zote zinamstahiki MwenyeziMungu bwana wa walimwengu wote.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari, Hizb ut Tahrir Kenya**




# Afisi Kuu ya Habari: Angazo Maalum "Baada ya Miaka Ishirini ya Vita vya Msalaba, Afghanistan Yaelekea Wapi?!"

Mnamo 07/10/2001 M, Amerika, kinara wa ukafiri, na mshirika wake Uingereza walianzisha vita vya kinyama dhidi ya Waislamu, waliishambulia kwa mabomu miji ya Afghanistan ya: Kabul, Kandahar, Jalalabad na mengineyo na makombora ya Tomahawk, na kurusha makombora na aina anuwai za silaha. zilitegemea anga, maji na ardhi za Waislamu ambazo ziliruhusiwa kwao na watawala wasaliti, haswa katika Pakistan na Uzbekistan. Hili liliendelea kwa wiki kadhaa mfululizo. Licha ya ujasiri mkubwa na ukakamavu wa hali ya juu ulioonyeshwa na Waislamu katika upinzani kwa wavamizi, kwa silaha hafifu walizokuwa nazo ikilinganishwa na nguvu za wavamizi, walakini ukali wa shambulizi la kikatili kutoka kwa wavamizi na usaliti wa watawala pambizoni mwa Afghanistan ulisababisha kuanguka kwa Afghanistan na kwenda mikononi mwa Amerika mnamo 2001 M.

Idadi ya vifo vya Waafghani katika robo karne iliyopita ilifikia zaidi ya milioni mbili, ikimaanisha kwamba idadi hii kubwa ya wahasiriwa ilishuka tu tangu uvamizi wa Urusi nchini Afghanistan mnamo 1979 M hadi baada ya uvamizi wa Amerika mnamo 2001 M. Kujitolea huku kukubwa kwa Afghanistan kulimalizika, na la kusikitisha sana, ni kuapishwa kwa Hamid Karzai kama mtawala kibaraka wa Amerika nchini Afghanistan.

Hati ya Bonn, ambayo ilianzisha katiba mpya ya Afghanistan mnamo 12/6/2001 M, ilisainiwa na Amerika kutoka Azimio la Baraza la Usalama Nambari 1883 kuiunga mkono, na katiba iliyomo kwenye waraka huo iliipa Amerika dori muhimu katika mavazi ya Umoja wa Mataifa katika kuamua mambo ya ndani na ya nje ya watu wa Afghanistan, na katika kusimamia kila jambo dogo na kubwa nchini Afghanistan, hati hiyo iliainisha uwepo wa Amerika katika kuanzishwa kwa chombo cha kikatiba, katika kuanzishwa kwa shirika la utumishi wa umma, katika kazi na mamlaka ya serikali, na katika mabadiliko yoyote yanayohusiana na sheria za kiutaratibu za taasisi zote za serikali, na katika ufuatiliaji wa tekelezaji wa nyanja zote za makubaliano, ikimaanisha kwamba Amerika imejiweka yenyewe kama mtawala halisi wa dola hii hadi atakapo Mwenyezi Mungu. Na hili ndilo linalodhihirisha siri za Amerika kwamba nia ni kulitawala eneo la Kiislamu, na wala sio kuwepo utawala (huru) kama inavyodai, bali kwamba vita vyake, ambavyo ilivitangaza kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi, sio chochote isipokuwa mlango wa vita vya msalaba dhidi ya Uislamu na Waislamu, kukaza udhibiti juu ya nchi yao, na kuutenga Uislamu na maisha yao kama walivyofanya na wanafanya nchini Afghanistan na Iraq, na kama ilivyoandikwa katika mradi wao (Mashariki ya Kati Kuu). Ni vita vya msalaba ambavyo vilivyofichuliwa na amali za jeshi, kisiasa na kielimu zilizofanywa na Amerika ambapo zililipuka katika nchi za Kiislamu. Hakika, Bush Mwana alizifichua tangu siku za mwanzo za matukio ya 9/11, katika hotuba yake tarehe 16/09/2001, ambapo alitangaza kwamba vita vyake dhidi ya ugaidi ni vita vya msalaba, na haikuwa imepita ila siku nne tu tangu mlipuko huo mkubwa, ambazo hazitoshi kukamilisha uchunguzi wa tukio ambapo haiwezi hata kufikia ushuri yake, ambapo inaonyesha kile kilichofichwa katika hazina ya wanasiasa wa Amerika dhidi ya Uislamu na Waislamu. Na ingawa aliviita (vita vya msalaba) kwa kuwakusanya maadui wa Uislamu pambizoni mwake, aliwaleta Waislamu pamoja kumpinga. Na huu ndio upinzani nchini Afghanistan, ulioilazimisha Amerika kurudi nyuma na kutafuta njia mbadala nchini Afghanistan. Katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita, vikosi vya Amerika, pamoja na vikosi vya kimataifa (ISAF) na uongozi wa NATO, havikuweza kupanua ushawishi wa uvamizi (kikamilifu) isipokuwa tu katika mji mkuu, huku maeneo yote ya Afghanistan nje ya Kabul yakisalia mandhari ya silaha operesheni za kisilaha ambazo hazikukoma hata siku moja baada ya uvamizi wa Amerika wa Afghanistan.

Hasara ambazo Amerika ilipata wakati wa uvamizi wake wa Afghanistan zinathibitisha kwamba Amerika ilikuwa

*Endelea... UK 4*


Email: info@uqab.or.ke

ikiondoka Afghanistan ikiburuta mkia wa kushindwa bila ya kutoka na mazungumzo ambayo yangeihifadhi kutokana na ushawishi ambao haingeweza kuufikia ndani ya vita!

**Na sisi katika Hizb ut Tahrir tunatambua kwamba katika Taliban kuna ndugu ambao ni wakweli wenye ikhlasi basi ni kwa watu hawa ndio tunawaelekea kwa kuwaambia:**

1- Sahihisheni jambo hilo na muache kujadiliana na Amerika, ili msiiwezeshe Amerika kufikia lile ambalo haingeweza kulifikia katika vita…

2- Na kinaikeni kuwa kadhia kuu ya Waislamu ni kuregeshwa kwa Khilafah baada ya kutoweka kwa muda mrefu, kwani ni faradhi ya Mwenyezi Mungu (swt) na utiifu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw)...

3- Na jueni kuwa kushiriki katika utawala wa mchanganyiko wa Uislamu na usekula haukubaliki na Mwenyezi Mungu, kwani Al-Qaqiy Al-Aziz hakubali chochote isipokuwa kizuri ...

Hii ndio haki ﴿فَمَاذَا بَعْدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ﴾ **"Na kipo kitu gani baada ya haki, isipokuwa upotovu tu?"** [Yunus: 32]. Na kufuata haki ndio kutakakoikoa Taliban, nchi hii, na watu wake, na Waislamu wote ... Hivi ndivyo Hizb ut Tahrir anakushaurini, kama tulivyokushaurini mwanzoni mwa utawala wenu kwa kutangaza Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume. Mkakataa kisha mkajua kuwa mumekosea kwa kukataa huko kama ilivyo pokewa kutoka kwa Mulla Omar Mwenyezi Mungu amrehemu katika mojawapo ya vikao vyake lakini baada ya kupita zama ... Sisi hapa tena tunaikariri naswaha je, yupo wa kuitikia?

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ
يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ﴾

**"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa."** [Al-Anfal: 24].

**Ijumaa, 20 Dhu al-Hijjah 1442 H**
**sawia na 30 Julai 2021 M**


Email: info@uqab.or.ke

# HABARI NA MAONI: AU kama Mtangulizi wake OAU ni Zana ya Kikoloni ambayo ya Muhalalisha Muuaji na Mvazi Umbile la Kiyahudi la 'Israel'

**Habari:**

Mnamo Alhamisi, 22 Julai 2021 Waziri wa Kigeni wa Israel Yair Lapid alitangaza kwamba Israel imejiunga na Muungano wa Afrika (AU) kama dola mtazamaji. Alisema kuwa Alhamisi ilikuwa ni siku ya sherehe kwa mahusiano ya Israel na Afrika, akitaja kuwa hivi sasa Israel ina mahusiano na nchi 46 za kutoka Afrika. Baada ya tangazo hilo kuthibitishwa na Mwenyekiti wa Tume ya Muungano wa Afrika (AUC), Moussa Faki, lilisababisha patashika kubwa huku Algeria, Misri, Libya, Tunisia, Mauritania, Comoros na Djibouti waliwasilisha upingaji wao wa hatua hiyo iliyochukuliwa na mwenyekiti wa AUC. Barua yao ilitiwa saini na Jordan, Kuwait, Qatar, Palestina na Yemen, na kuongezea uwakilishi wa Ligi ya Kiarabu. Upande mwingine, Botswana na Namibia zilizipinga maamuzi hayo ilhali serikali ya Afrika Kusini ilitoa taarifa ikisema kuwa AUC ilichukuwa maamuzi hayo kibinafsi pasina kuwataka ushauri wanachama wake. (The Star, 07/08/2021)

**Maoni:**

Patashika hiyo ni njama tu ya nchi hizo kuokoa sura zao mbele ya raia wao. Lakini kiuhalisia wote ni washirika katika uhalifu pamoja na AU kwani sera yake msingi ni ile ya suluhisho la dola mbili! Kama ilivyothibitishwa na kauli ya mwenyekiti wa AUC kwamba ana matumaini kuwa kuidhinishwa kwa 'Israel' kuwa dola mtazamaji itazidisha kasi ya mchakato wa AU ya kutimiza msingi wa dola mbili na kurudisha amani baina ya dola mbili na watu kutoka pande mbili!

Umbile la Kiyahudi 'Israel' ni kivuli tu ambacho kipo kama natija ya usalama kinaopewa na mataifa iliyokizunguka. Mataifa hayo yanatawaliwa na watawala vibaraka wa wakoloni ambao wameuza roho zao kwa wakoloni Wamagharibi walioko Washington, London na Paris. Hivyo basi, sera zao hutegemea maslahi ya mabwana zao. Kupinga kwao sio chochote bali ni porojo ili kuwahadaa watu wa Palestina kwamba wana uungwaji mkono kutoka kwao! Badala yake wao ndio wanaopiga njama na kuwachimbia makaburi!

Palestina ni suala la Kiislamu ambalo linahitaji dola huru ya Kiislamu ya Khilafah iliyosimamishwa kwa njia ya Utume ili kuyaunganisha majeshi yake na kuikomboa Al-Aqsa na ardhi nyingine za Waislamu. Kukosekana kwa Khilafah kunatoa nafasi kwa zana za kikoloni kama vile AU na mfano wake ili kuhalalisha kuwepo kwa muuaji na mvamizi umbile la Kiyahudi 'Israel.' Ama kuhusu Afrika ni shamba la kikoloni tu, watawala wake vibaraka ni mameneja katika shamba la kikoloni na raia wake ni wafanyakazi wa kikoloni.

Haishangazi, kuona kuwa Uingereza, Amerika, Ufaransa n.k ni dola watazamaji katika AU! Wanadhamini miradi yake, wanachora sera zake na kujenga miundombinu yake kwa gharama kubwa ili wapate nini?! Hakika, inathibitisha ule msemo, 'mbwa ni mtumwa kwa bwana wake.' Madhara yasiyo hesabika yanayo sababishwa na dola za kikoloni za Kimagharibi barani Afrika and duniani kwa upana yameanzia katika ukandamizaji wa kifikra hadi uporaji wa rasilimali. Hivi sasa Amerika iko safu ya mbele kuongoza katika mashambulizi dhidi ya kusimamisha tena dola huru ya Kiislamu, Khilafah.

Minong'ono ya mabadiliko haiwezi kupuuziliwa mbali hususan sasa hivi ambapo kuanguka kwa utawala wa Amerika kuko karibu. Matukio yanayotokea ndani ya Amerika, inayojidai kuwa ni ngome ya demokrasia inafichua kufeli kikamilifu kwa mungu wa kidemokrasia. Hivyo basi, dola kuu mbadala iko karibu kuchipuza ili kuwakomboa wanadamu kutoka katika ukandamizaji na maangamivu ya mfumo wa Kimagharibi wa kisekula wa kirasilimali na walinganizi wake. Hakika, mbadala sio nyingine bali ni Khilafah iliyosimamishwa kwa njia ya Utume.

Kwa sababu hiyo, sasa ndio wakati wa kujiunga na kufanyakazi ya mradi wa #TurudisheniKhilafah. Mradi ambao lengo lake ni kuwakomboa wanadamu kutoka katika kuabudu viumbe hadi kumuabudu Muumba wao – Mwenyezi Mungu (swt). Mradi ambao utaitikia vilio vya walioko Al-Aqsa, Kashmir, Syria, Yemen, Afghanistan nk. Kurudisha maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha tena Khilafah kutaleta usalama, amani, utulivu na ustawi wa kweli ambao unahitajika kwa dharura mno. Kwani serikali ya Khilafah itatekeleza kwa ukamilifu nidhamu za Kiislamu zinazochipuza kutoka katika Shari'ah.

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Msoto wa Kiuchumi: Uislamu Ndio Jibu

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

Mwenyezi Mungu (swt) asema: وَٱبۡتَغِ فِيمَآ ءَاتَىٰكَ ٱللَّهُ ٱلدَّارَ ٱلۡأٓخِرَةَۖ وَلَا تَنسَ نَصِيبَكَ مِنَ ٱلدُّنۡيَاۖ وَأَحۡسِن كَمَآ أَحۡسَنَ ٱللَّهُ إِلَيۡكَۖ وَلَا تَبۡغِ ٱلۡفَسَادَ فِي ٱلۡأَرۡضِۖ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ ٱلۡمُفۡسِدِينَ **"Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi."** [28. Al-Qasas: 77] Kwa kuongezea Mtume (saw) alituonya kuhusu namna ya tunavyo chuma mali na kuitumia: «لاَ تَزُولُ قَدَمَا ابْنِ آدَمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مِنْ عِنْدِ رَبِّهِ حَتَّى يُسْأَلَ عَنْ خَمْسٍ عَنْ عُمْرِهِ فِيمَا أَفْنَاهُ وَعَنْ شَبَابِهِ فِيمَا أَبْلاَهُ وَمَالِهِ مِنْ أَيْنَ اكْتَسَبَهُ وَفِيمَ أَنْفَقَهُ وَمَاذَا عَمِلَ فِيمَا عَلِمَ» **"Miguu ya wanadamu haitoondoka mbele ya Mola wake Siku ya Kiyama, mpaka atakapoulizwa mambo matano: kuhusu uhai/umri wake na aliufanyia nini, kuhusu ujana wake na aliutumia katika nini, kuhusu mali yake na namna alivyoichuma na kuitumia na alikifanyia nini alichokuwa anakijua."** [Tirmidhi]

Wanadamu wamerithishwa mali za dunia na Mwenyezi Mungu (swt) kwa kuwa Yeye ndiye Muumba wa ulimwengu, mwanadamu na uhai. Hivyo basi, kufaulu katika uchumaji na matumizi ya mali hutakiwa kuwa kwa mujibu wa muongozo wa Muumba. Kinyume chake kutashuhudiwa majanga na ufisadi wa kupindukia kama hali ilivyo sasa duniani kote. Leo ulimwengu unatawaliwa na mfumo wa kisekula wa kirasilimali. Mfumo ambao umechipuza kutoka katika akili za wanadamu. Nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali inatambua tatizo la kiuchumi ni uhaba wa rasilimali. Hivyo basi, nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali humaanisha kutatua tatizo la kukidhi mahitaji ya mwanadamu na njia za kukidhia mahitaji hayo kwa mujibu wa mfumo wa kirasilimali. Kwa maana hiyo msingi wa nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali ipo kwa ajili ya kuweka mipango na kuiboresha ili kutatua tatizo la uhaba wa rasilimali. Huku mahitaji hayo yakizingatia uhuru usiokuwa na mipaka kwa mujibu wa nidhamu huria ya kijamii!

Nidhamu ya kiuchumi ya kirasillimali ipo kwa ajili ya kuwapora watu mali zao kupitia utozaji ushuru uliopewa majina tofauti tofauti. Na kuongezea kupitia mikopo ya riba ambayo huwazidishia watu umasikini na tabu katika maisha. Nchi hususan za ulimwengu wa tatu huchukua mikopo ya riba ambayo huwa na masharti magumu na yenye kuleta madhara makubwa kwa raia wao. Masharti hayo huwa ni kutokana na kushurutishwa na taasisi za kifedha za dunia kama vile Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Taasisi hizi hushirikiana na benki kuu za nchi husika katika kuwatia vitanzi na kuvikazanisha katika shingo za raia. Hili hupelekea katika kuzidishwa ushuru kwa bidhaa na huduma, na kutozwa ushuru bidhaa na huduma ambazo awali zilikuwa hazitozwi na kufutiliwa mbali ruzuku zote au baadhi, malipo ya riba kuzidi kwa kutegemeza malipo ya mikopo kwa sarafu ya dolari ($) n.k. Hivyo gharama ya maisha hupanda na uwezo wa raia wengi kununua bidhaa na huduma huzidi kuporomoka kwa kasi. Ilhali ukuwaji wa uchumi hupimwa kwa kutegemea faida na hasara ya makampuni na sio uwezo wa raia kukidhi mahitaji yao!

Mfumo wa Uislamu ambao unachipuza kutoka kwa Muumba wa viumbe, Mwenyezi Mungu (swt). Nidhamu yake ya kiuchumi inatambua tatizo la kiuchumi ni usambazaji wa rasilimali. Hivyo basi, nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu humaanisha namna ya kusambaza mali, namna ya kuimiliki na namna ya kuitumia kwa mujibu wa mfumo wa Kiislamu. Kwa maana hiyo msingi wa nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu ni kwenda mbio kuifanyia kazi Shari'ah (Qur'an na Sunnah) ikiwa ni pamoja na kuweka mipango na kuiboresha ili kutatua tatizo la usambazaji wa rasilimali. Kwa kuongezea sera ya kiuchumi ya Kiislamu inadhamini watu binafsi kukidhi mahitaji yao msingi ikiwemo kupata chakula, mavazi na makaazi na pia kukidhi mahitaji ya kimujtama ikiwemo elimu, usalama na matibabu. Kwa kurudisha tena maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha dola ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume ndio njia pekee ya kuitekeleza nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu. Mapato na matumizi ya Khilafah yamefungwa na Shari'ah na hayajumuishi utozaji raia ushuru wala kuchukuwa mikopo ya riba kwa ajili ya kuwasimamia watu au kuendesha serikali. Utozaji ushuru na mikopo ya riba imeharamishwa katika Uislamu.

Msoto wa kiuchumi unaoshuhudiwa duniani kote hivi sasa suluhisho lake ni watu kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume. Kufanya hivyo kutapatikana mafanikio na maendeleo ya kiuchumi ya kweli.



# UCHUMI MUOVU WA KIBEPARI NDIO CHANZO CHA MSOTO

Ni wazi kuwa uchumi ndio uti mgongo wa maisha ya wanadamu na hupelekea udharura wa kuweko utaratibu wa kuendesha ukuzaji na usambazaji wa rasilimali (utajiri) katika jamii. Mfumo wa kiuchumi leo ni ubepari/ urasilimali uliotungwa na msomi wa kimagharibi Adam Smith anayetambulika 'Baba wa mfumo wa Kirasilimali'. Ubepari humaanisha kwamba biashara, viwanda na vitegauchumi vyote vinamilikiwa na watu binafsi waliojaa uchu na tamaa ya kujirundikizia mali pasina na kujali thamani ya utu. Matokeo yake, utajiri hubakia na kumilikiwa na kipote cha mabepari huku jumla ya watu wakisota kila siku.

Urasilimali ndio chanzo halisi cha msoto wa kiuchumi duniani kote, hii inarudia falsafa yake katika kuainisha tatizo msingi la kiuchumi na katika kulisulihisha kwake; nayo ni kudai kwamba kuna uhaba wa bidhaa na huduma katika kukimu mahitaji ya wanadamu. Kukabiliana na tatizo hili, wakoloni wakirasilimali hudai ni kupitia uzalishaji wa bidhaa na huduma! Kwa msingi huu, Ubepari ukafanya uzalishaji wa bidhaa na huduma ndio kipaumbele huku ukipuuza usambazaji wake. Natija yake ikawa utajiri wa nchi ndio mizani ya ukuaji wa kiuchumi hata kama jumla ya wananchi wa kawaida wapo kwenye lindi la umasikini.

Mabwenyenye wa kirasilimali wamepagawa na uchu wa kupata faida ya kupindukia na hawatukuzi lolote ila maslahi ya kiuchumi kwao. Sifa hii ndio yenye kuathiri pia utendakazi wa serikali, sera za kiuchumi na hata siasa. Utekelezwaji wa mfumo huu wa utumwa mambo leo katika mashingo ya watu, umewazalishia maafa mengi ya kiuchumi kama inavyodhihirika kwenye suala la ajira. Kwa haya ndio, wafanyikazi wanaendelea kuhudumikia maslahi ya mabwenyenye huku wakiambulia patupu na hata mishahara huishia kuwa kijungumwiko.

Makucha ya urasilimali huingia ndani ya mfuko wa mlala hoi kwa kumlimbikizia zigo la ushuru katika kila bidhaa na huduma msingi. Kwa kuwa kila mwanadamu huhitaji bidhaa na huduma kwenye maisha ya kila siku, utozwaji wa ushuru moja kwa moja huzidisha dhiki ya maisha ya raia. Tunasema kuwa ushuru ni zigo kwa mlalahoi wala si kwa matajiri kwa sababu hautozwi kwa mali za matajiri bali ni kwa bidhaa na huduma. Na hata zile ziitwazo kodi za makampuni bado hazigusi utajiri wa wamiliki wa kampuni bali mara nyingi matajiri huweka hesabu ghushi.Hivyo inabainika kwamba katika mfumo wa kirasilimali utajiri huzunguka kwa watu wachache huku wengi wakibakia kuwa watumwa wasomudu kukimu hata mahitaji msingi. Utumwa huu wa Kirasilimali ni katili zaidi hata kuliko ule wa mabwenyenye wa kiquraishi kwani watumwa wa zama hizo walikuwa wakifadhiliwa malazi na chakula.

Uislamu kwa upande wake nao ni mfumo kamili wa kimaisha unajumuisha utaratibu wa kiuchumi/nidhamu. Uchumi wa Kiislamu huangazia vipengele vitatu; njia za kumiliki mali, matumizi na ugavi. Tatizo la kiuchumi katika mfumo wa kiislamu linalopaswa kutatuliwa sio uhaba wa bidhaa na huduma bali ni usambazaji. Kwa maana hii, suluhisho la tatizo ya kiuchumi ni usambazaji wa mali wala sio kupitia uzalishaji wa mali. Mfano hai ni kuwa Kenya kiuhalisia ni yenye utajiri mkubwa,lakini kwa sera mbovu za usambazaji,watu hufa njaa maeneo mengi ya nchi huku baadhi ya maeneo vyakula vinatupwa! Kwa uhalisia huu,umasikini wa watu hautokamani na uwezo wa uzalishaji wa mali bali ni usambazaji wake kukidhi mahitaji msingi ya wanadamu. Katika kutilia mkazo Uislamu ukaharamisha urundikizaji wa mali na ukiritimba. Mwenyezi Mungu (Swt) anasema

وَالَّذِينَ يَكْنِزُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلاَ يُنفِقُونَـهَا فِي سَبِيلِ اللهِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيم

**Na wale wanaokusanya dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njiya ya MwenyeziMungu wape habari za adhabu inayoumiza.** [TMQ 9:34]

Ama suala la ajira, Uislamu umefafanua kwa kina suala hili, awali ya yote ni kulifungamanisha kwake na ibada. Kazi yoyote ile hayaingaliwi kwa msingi wa manufaa ni kwa kuzingatia uhalali na uharamu kwani ndio vipimo katika matendo ya wanadamu. Kiislamu, mishahara au malipo ya juhudi ya mfanyikazi haifungamanishwi na manufaa ya mwajiri bali ni kwa kulingana na manufaa yanayozalishwa na yule mfanyikazi. Kwa maana haya inabainika kuwa ajira katika Uislamu ni njia ya kujikwamua kikweli na msoto wa kiuchumi wala sio utumwa mambo leo kama ilivyo ndani ya urasilimali. Fauka ya haya, mapato ya kuendesha serikali kwa mujibu wa Uislamu sio utozwaji ushuru bali ni kuegemea mali/utajiri ulioko kwa mazingatio ya usambazaji.kwa mfano pato la zaka ya mali,huchukuliwa asilimia 2.5 kwa mali iliyofikia kiwango maalum kwa muda maalum.

Enyi Waislamu na Wasokuwa Waislamu, kwa hakika msoto wa kiuchumi unaoshuhudiwa ni dalili tosha ya kufeli kwa mfumo wa kiuchumi wa Kibepari. Wakati ni sasa wa kuitikia mwito wa mabadiliko msingi itakayowapelekea kupata mafanikio ya hapa duniani na kesho akhera. Mabadiliko haya ni kuulingania Uislamu kuwa mfumo pekee ulio na nidhamu ya kikweli ya kiuchumi,kisiasa na kijamii ili uongoze watu katika nyanja zote maishani kupitia kusimamishwa tena kwa Khilafah katika moja wapo ya nchi katika ulimwengu wa Kiislamu.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱسْتَجِيبُواْ لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ

**Enyi Mlioamini Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume wake anapokuiteni katika yale yatakayokupeni uhai mzuri (wa duniani na Akhera.** [TMQ 8:24]

**Hizb ut-Tahrir Kenya**
**27 Dhul-Hijja 1442 A.H**
**06 August 2021 C.E**


Email: info@uqab.or.ke

# Athari za Kisiasa nchini Afghanistan




**Swali:**

Mnamo 17 Julai 2021, mazungumzo ya ngazi ya juu yalitangazwa nchini Qatar kati ya ujumbe miwili wa ngazi ya juu, wawakilishi saba kutoka Taliban na ujumbe wa wanachama saba wa serikali [Afghanistan], kujadili maswala muhimu kati yao, baada ya Rais wa Amerika kutangaza mnamo Julai 8, 2021 kwamba uondoaji wa vikosi vyake kutoka Afghanistan utakamilika ifikapo tarehe 31 Agosti, na kuusongeza mbele kutoka tarehe ya makataa ambayo alikuwa ameweka hapo awali. Mafanikio ya harakati ya Taliban yamezingatiwa katika maeneo makubwa ya Afghanistan, yamefikia asimilia 85, kama ilivyotangazwa na harakati hiyo ... Kwa mujibu wa Mkataba wa Doha wa 2020, mazungumzo kati ya harakati hiyo na serikali yana jukumu la kufikia mbinu ya ugavi wa mamlaka ya kisiasa. Je! Taliban watachukua udhibiti wa serikali au watagawanya tu madaraka? Je! Amerika kweli itaondoka au ushawishi wake utaendelea?

**Jibu:**

Ili kufikia rai nzito zaidi juu ya mambo haya, tunazingatia yafuatayo:

1. Wakati Amerika ilipoanza kupanga kwa umakini kujiondoa kwake Afghanistan, tangu mwishoni mwa 2010 na mwanzoni mwa 2011, Amerika ilitaka kuanza mazungumzo na viongozi wakuu wa Taliban kwa umakini, na Pakistan kama msimamizi katika mazungumzo haya. Amerika ilijionyesha kubadilika kwa Taliban, kiasi ya kuwa mnamo 2014 mazungumzo yalisababisha kubadilishana kwa wafungwa. Wafungwa watano wa Taliban kutoka Ghuba ya Guantánamo waliachiliwa huru kwa mbadala wa Taliban kumwachilia huru Mmarekani mmoja, Private Beaudry Robert "Bowe" Bergdahl, ambaye alikuwa anashikiliwa mateka na Taliban ... Halafu maendeleo katika mazungumzo yalishika kasi chini ya wanaume wawili waliohudumu kwa muda mrefu katika mamlaka husika walizowakilisha. Mnamo 5 Septemba 2018, Zalmay Khalilzad aliteuliwa kama Mwakilishi Maalum wa Amerika wa Upatanishi wa Afghanistan, aliyepewa jukumu la kumaliza uvamizi wa kijeshi wa Amerika nchini Afghanistan. Ndani ya miezi miwili ya kuteuliwa kwa Khalilzad, tarehe 22 Oktoba 2018, Pakistan ilimwachilia huru Mullah Abdul Ghani Baradar, ambaye alikuwa anazuiliwa nchini Pakistan tangu kukamatwa kwake huko Karachi, kufuatia uvamizi wa tarehe 8 Februari 2010. Baada ya kuachiliwa huru, Mullah Baradar aliteuliwa kuwa mkuu wa afisi ya kidiplomasia ya Taliban jijini Doha. Habari za Kiarabu za BBC ziliripoti mnamo 25 Februari 2019, kwamba, "Jina la Mullah Baradar lilikuja juu ya orodha ya wafungwa ambaye harakati hiyo ilitaka kuachiliwa kwake, katika

*Endelea... UK 9*


Email: info@uqab.or.ke

mazungumzo yake mfululizo na maafisa wa Amerika na serikali ya Afghanistan, hadi hatimaye kuachiliwa huru mnamo Oktoba 2018, baada ya mazungumzo yaliyopatanishwa na Qatar." Ni hawa wanaume wawili ambao walicheza dori kubwa katika mazungumzo ya yaliyofuatia.

2. Mazungumzo haya yalimalizika kwa Mkataba wa Doha wa tarehe 29 Februari 2020, jambo ambalo lilikuwa maarufu zaidi liliripotiwa na BBC News Arabic, ambayo ilisema, "Maafisa wa Amerika na Afghanistan walitangaza kuwa Amerika na washirika wake wa NATO wataondoa vikosi vyao kutoka Afghanistan ndani ya miezi kumi na nne, ikiwa Taliban itatimiza majukumu yao, chini ya makubaliano ambayo yalitiwa saini nchini Qatar jijini Doha leo. Tangazo hilo lilikuja katika taarifa ya pamoja ya Amerika na Afghanistan iliyotolewa jijini Kabul. Rais Donald Trump alisema ilikuwa "safari ndefu na ngumu" nchini Afghanistan. "Ni wakati sasa baada ya miaka hii yote kurudisha watu wetu nyumbani," alisema." BBC iliongeza, "Zaidi ya wanajeshi 2,400 wa Amerika waliuawa wakati wa mzozo huo."

3. Baada ya Makubaliano ya Doha, taarifa na mikutano ilikola kasi, licha ya kuendelea kwa mapigano, kwa viwango vya juu na vya chini.

CNN iliripoti mnamo 14 Aprili 2021 kwamba Joe Biden alitangaza, "Mimi sasa ni rais wa nne wa Amerika kusimamia uwepo wa vikosi vya Amerika nchini Afghanistan. Wawili wa chama cha Republican. Wawili wa chama cha Democtrats, aliendelea. "Sitapokeza jukumu hili kwa rais wa tano… Ni wakati sasa wa kumaliza vita virefu kabisa vya Amerika."

Biden kisha alitoa hotuba, ikifuatiwa na mkutano na waandishi wa habari uliopeperushwa kwenye runinga za Amerika na za kimataifa, mnamo 8 Julai 2021, akisema, "Tunavimaliza vita virefu kabisa vya Amerika ... Tulikwenda kwa sababu mbili: moja, kumleta Osama bin Laden... Sababu ya pili ilikuwa kuondoa al Qaeda… Tulitimiza malengo yote hayo - kwisha." Alisema pia kwamba, "Misheni yetu ya kijeshi nchini Afghanistan itahitimika mnamo 31 Agosti." Aliongeza, "Hatukwenda Afghanistan kujenga taifa. Na ni haki na jukumu la watu wa Afghanistan peke yao kuamua mustakbali wao na jinsi wanavyotaka kuendesha nchi yao." Biden pia alisema, "Na tunahitaji pia kuzingatia kuongeza nguvu msingi za Amerika kufikia mashindano ya kimkakati na China…. Tunapaswa kuishinda COVID-19… Tunahitaji kuanzisha desturi za kimataifa za mtandao ... Na tutakuwa imara zaidi…. endapo tutapigana vita vya miaka 20 ijayo, sio miaka 20 iliyopita."

Katibu wa Wanahabari wa Ikulu ya White House ya Amerika, Jen Psaki alisema kinaga ubaga, "hatutakuwa na wasaa "Misheni Imekamilishwa" katika suala hili. Ni vita vya miaka 20 ambavyo havijashindwa kijeshi." (Anatolia Arabic 8 Julai 2021), ikimaanisha kwamba Amerika haikupata ushindi nchini Afghanistan, licha ya miaka 20 ya kujaribu. Mnamo 2 Julai 2021, Amerika ilihamisha kambi yake muhimu zaidi na kubwa zaidi, Bagram, baada ya kufunga kambi nyenginezo hapo awali, ikimaliza kihakika vita vyake vya msalaba kabla ya tarehe rasmi iliyotangazwa na Rais Biden wa Amerika hapo awali, 11 Septemba, na kabla ya tarehe ya pili aliyoiweka, 31 Agosti.

Wakati huo, harakati ya Taliban ilipanua mashambulizi yake ya kijeshi na wilaya zikaanza kuanguka kaskazini, kusini, magharibi na kisha katikati. Kasi ya udhibiti wa harakati ya Taliban juu ya ardhi nyingi za Afghanistan ikawa isio na kifani, haswa kwenye mipaka ya nchi jirani, na pia kukamata kwao vivuko na nchi jirani. Shahabuddin Delawar, mwanachama wa timu ya mazungumzo ya Taliban jijini Moscow, alisema mnamo 9 Julai 2021, "asilimia 85 ya eneo la Afghanistan limeingia chini ya udhibiti (wa Taliban)," huku msemaji wa vikosi vya usalama vya Afghanistan, Ajmal Omar Shinwari, akikataa vikali hili, akisema: "Hii sio kweli. Mapigano yanaendelea katika maeneo mengi." (Agence France-Presse Arabic, 11 Julai 2021). Lakini, ujumbe wa Taliban uliahidi, "kutoingilia kati nchi jirani na nchi za kirafiki"… Yeye (Delawar) alisema kuwa ziara yake jijini Moscow inakusudia kutoa habari zote kuhusu kile alichokiita "Imarati ya Kiislamu." Aliongeza kuwa Taliban haitaruhusu upanuzi wa ISIS nchini Afghanistan na akasisitiza kuwa harakati hiyo itapambana nayo. Ujumbe huo pia ulithibitisha kwamba harakati hiyo inafanya mazungumzo na wawakilishi wa kijamii kufafanua muundo jumla wa dola na kwamba kazi hii inakaribia kukamilika… na kwamba harakati hiyo hailengi kunyakua mamlaka kikamilifu." (Al-Jazeera Arabic 9 Julai 2021).

4- Kisha ikatangazwa mnamo 17 Julai 2021, kwamba, "Pande hizo mbili za mzozo nchini Afghanistan zilikubaliana leo, Jumamosi, jijini Doha, kuunda kamati yenye wajumbe kumi na nne, kwa njia ya usawa, kujadili ajenda ya mazungumzo, ambayo yatajadili mambo ambayo yangali hayajatatuliwa. Mwandishi wa Al-Jazeera alinukuu chanzo katika mazungumzo ya Afghanistan jijini Doha, akisema kwamba kikao cha ufunguzi wa mazungumzo kilimalizika katika mazingira chanya. Raundi mpya ya mazungumzo kati ya serikali ya Afghanistan na harakati ya Taliban imezinduliwa leo katika mji mkuu wa Qatar, Doha na raundi hii inajadili mambo na maswala yaliyoelezewa kuwa ya muhimu. Abdullah Abdullah, Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Upatanishi wa Kitaifa la Afghanistan na mkuu wa ujumbe wa serikali, alisema kuwa kufanikiwa kwa amani nchini kunahitaji mnyumbuko kwa pande zote mbili, na kuongeza kuwa uwanja sasa mzuri kwa amani. Kwa upande wake, mkuu wa afisi ya kidiplomasia ya Taliban jijini Doha, Mullah Abdul Ghani Baradar, alisema kuwa watafanya kila wawezalo kufikia matokeo mazuri katika mazungumzo ya amani ya Afghanistan ambayo yameanza leo jijini Doha." (Chanzo: Al-Jazeera Arabic na Mashirika).

***Endelea... UK 10***

5. Kisha kamati ikakamilisha kazi yake leo, 18 Julai 2021, na taarifa ya pamoja ambayo ilitolewa kuhusu mkutano huo. Iliarifiwa kuwa, "Mwandishi wa Al-Jazeera jijini Doha alisema kuwa wajumbe wa serikali ya Afghanistan na harakati ya Taliban walifikia makubaliano juu ya taarifa ya mwisho ya pamoja ya mazungumzo yao yanayoendelea, jijini Doha na upatanishi wa Qatar, kufanya mkutano mwingine hivi karibuni kwa mkondo wa Doha. Pande hizo mbili zilikubaliana kuharakisha mazungumzo ili kupata suluhu ya haki kwa mzozo ambao umekuwa ukiendelea nchini kwa miongo kadhaa. Taarifa ya pamoja ya ujumbe wa serikali ya Afghanistan na Taliban iliainisha makubaliano ya kuharakisha mazungumzo ili kufikia suluhisho la haki, wakijitolea kufanywa kwa kiwango cha juu hadi suluhu ifikiwe. Kwa hivyo, ilimaliza raundi ya pili ya mazungumzo ya amani ya Afghanistan, ambayo yanalenga kufikia suluhu ya kisiasa ambayo inapelekea katika amani nchini, baada ya miongo kadhaa ya vita. Chanzo kimoja katika ujumbe wa Taliban kilisema kwamba harakati hiyo iliwasilisha pendekezo ambalo linajumuisha hatua za kujenga imani kati yake na serikali, kupitia kuwaachilia huru wafungwa pande zote mbili na kutangaza usitishaji wa mapigano katika kipindi cha Idd al-Adha ....” (Chanzo : Al Jazeera na mashirika.)

6- Inafaa kutaja msimamo wa dola mashuhuri ambazo Amerika huzitumia kwa uchangamfu katika mazungumzo na Taliban nchini Afghanistan:

a. Pakistan: Pakistan ndio iliyoishinikiza Taliban kufanya mazungumzo na Amerika mnamo 2018. Zalmay Khalilzad aliishukuru Pakistan kwa kuwezesha safari ya Taliban kwa ajili ya mazungumzo jijini Doha, huku Waziri wa Ulinzi wa Amerika, Lloyd James Austin III, katika mazungumzo ya simu mnamo 21 Machi 2021 na Mkuu wa Jeshi la Pakistan, Jenerali Bajwa, "alitoa shukrani kwa kuendelea kwa Islamabad kuunga mkono mchakato wa amani wa Afghanistan." (Mkuu wa Pentagon Asifu dori ya Pakistan katika Mchakato wa Amani wa Afghanistan, Jarida la Al-Fajr, Machi 23, 2021). Maafisa wakuu wa jeshi na viongozi wa kisiasa nchini Pakistan wamecheza dori kubwa katika mkakati wa Amerika kwa Afghanistan.

Kwa hivyo, dori ya Pakistan ni dori kubwa, sasa na kihistoria. Harakati ya Taliban ya Afghanistan ina asili ya Pakistan, kiasi ya kuwa ISI ya Pakistan na mashirika mengine ya kijasusi yana ushawishi wao nchini Afghanistan, huku wakiwa na mawasiliano na wanaume wao ndani ya Taliban. Hivyo basi, Amerika inategemea sana dori ya Pakistan.

b- Uturuki: Kama ilivyofanya nchini Syria na Libya, Uturuki inaelekea Afghanistan, ili kusaidia malengo ya sera za kigeni za Amerika. Wakati wa mkutano wa kimataifa katika hoteli ya kitalii ya Uturuki ya Antalya, Waziri wa Mambo ya nje wa Uturuki, Mevlut Cavusoglu, alipendekeza kuendeshwa na kulindwa kwa Uwanja wa Ndege wa Kabul na Uturuki ... Washington ilikubali kujitolea kwa Ankara kucheza dori muhimu katika kuulinda Uwanja wa Ndege wa Kabul, kufuatia mkutano wa Biden na Erdogan jijini Brussels mwezi uliopita. Amerika inataka Uturuki kutekeleza jukumu la ulinzi katika uwanja huo wa ndege, huku ikiwa bado inadumisha wanajeshi wake takriban 500 karibu na uwanja huo wa ndege wa kimataifa. Katika hotuba yake ya tarehe 8 Julai 2021, Biden aliashiria hilo, akisema, "tunashirikiana kwa karibu na washirika wetu wa kimataifa ili kuendelea kuulinda uwanja wa ndege wa kimataifa jijini Kabul." Erdogan alisema, "Tumeamua pamoja na Amerika na NATO mipango ya misheni ya mustakbali na kile tunachokikubali na kile tusichokikubali. Tuliibua suala hili wakati wa mikutano ya NATO, wakati wa mkutano wangu na Biden na wakati wa majadiliano kati ya wajumbe wetu. Tutatekeleza operesheni hii nchini Afghanistan kwa njia bora zaidi.” (Al Jazeera Arabic, 9 Julai 2021). Iliripotiwa mnamo 2 Julai 2021, kuhusu Msemaji wa Rais wa Uturuki, Ibrahim Kalin, "Uturuki itaendelea kulinda uwanja wa ndege wa Kabul hata baada ya wanajeshi wa NATO kuondoka Afghanistan msimu huu wa kiangazi, (Al-Awsat, 3 Julai 2021), huku harakati ya Taliban ikikataa uwepo wa Uturuki. Taliban ilitangaza katika taarifa moja, "Kukataa kwake kuviweka vikosi vya Uturuki nchini Afghanistan baada ya kuondolewa kwa vikosi vya kimataifa vinavyoongozwa na Amerika nchini na kusisitiza kuwa uamuzi kama huo ni wa kulaaniwa. Uamuzi huo wa uongozi wa Uturuki umeshauriwa vibaya, ni ukiukaji wa ubwana wetu na heshima ya eneo na dhidi ya maslahi yetu ya kitaifa… Na tunawasihi vikali maafisa wa Uturuki kubadili maamuzi yao kwa sababu ni mabaya kwa nchi zote mbili." (Al Jazeera, 13 Julai 2021)

c. Asia ya Kati: Amerika imekuwa ikiongea na viongozi katika Asia ya Kati juu ya kuweka upya baadhi ya vikosi vyake huko. Jarida la 'The New York Times' liliripoti kwamba maafisa wa Amerika wamekuwa wakiwasiliana na mamlaka za Kazakh, Uzbek na Tajik kuhusu uwezekano wa utumiaji wa kambi katika eneo hilo. Katibu wa Waziri wa Kigeni wa Amerika, Anthony Blinken, alisema katika msururu wa nukuu za tweets kwamba alizungumza mnamo Aprili 22 na mawaziri wa kigeni wa Uzbekistan na Kazakhstan juu ya utumiaji wa kambi za kijeshi wa Amerika na vikosi vyengine vya NATO. Jarida hilo la 'The New York Times' lilisema kwamba, "Droni, mabomu ya masafa marefu na mitandao ya kijasusi itatumiwa na Amerika na washirika wa Kimagharibi katika juhudi za kuzuia Afghanistan kujitokeza tena kama kambi ya kigaidi." (Jarida la 'The New York Times' 27 Aprili 2021)

7- Kwa kuzingatia hayo yaliyotajwa juu, ni wazi kuwa:

a- Mazungumzo yanayoendelea hayatapelekea kuondolewa kwa Amerika kutoka Afghanistan, lakini badala yake yatapelekea katika uhadaifu, kiasi ya kuwa Amerika inatoka kwa mlango wa mbele, na kuingia

***Endelea... UK 11***

kupitia mlango wa nyuma, ambao unalindwa na vibaraka na wafuasi nchini Pakistan, Uturuki na Iran na wale wanaoduru pamoja nao miongoni mwa vibaraka wa Amerika ndani ya Afghanistan yenyewe, huku dola hizi zikicheza dori muhimu kwa ajili ya kudumisha ushawishi wa Amerika nchini Afghanistan…

b - Ama Qatar, inaandaa mazingira ya mazungumzo kwa malengo mawili: la kwanza, ni kwa ajili ya kubadilishana na Amerika kuondoa kizuizi cha Saudi au "kuzingirwa" dhidi yake, na hii ndio imekuwa hali ... haswa baada ya Makubaliano ya Doha kuhitimishwa mnamo 29 Februari, 2020 wakati wa utawala wa Trump ... na lengo la pili ni kwamba Qatar, Waingereza wakiwa nyuma yao, wameanza kutumia mawasiliano yao na Taliban kuiaibisha Amerika. Hii ni kutoka kwa upande wa kuingilia kwa makusudi, kwani wanatoa msaada wa kifedha kwa harakati ya Taliban na kupeana afisi ya kidiplomasia pamoja na jukwaa la vyombo vya habari kwao, kiasi ya kuwa Amerika baadaye ihitaji dori ya Qatar kuwezesha mawasiliano yake na harakati ya Taliban... Na hivi ndivyo Waingereza wanavyojiweka kwenye picha. Na Waingereza hutumia hii kutumikia maslahi yao nchini Qatar na Ghuba, wakitumia fursa ya haja ya Amerika ya dori ya Qatar katika kuwezesha mawasiliano na Taliban ...

C - Kuingia kwa Taliban katika mazungumzo na Amerika na vibaraka wake katika serikali ya Afghanistan ilikuwa ni kosa kubwa sana ... Tunamwomba Mwenyezi Mungu (swt), Mwenye uwezo na nguvu, kuwalinda Waislamu nchini Afghanistan kutokana na uovu wao, kwani makafiri wakoloni wanajadili tu kufanikisha maslahi yao, kwa sababu ya dhurufu zinazowalazimisha. Yule anayechunguza dhurufu hizi kwa makini zinazoilazimisha Amerika sasa atazione kuwa dhahiri. Kwa hivyo, kwa kila mwenye akili, husikiza na kuzingatia:

Kwanza: Kuibuka kwa China kama nguvu ya kijeshi na kiuchumi katika karne hii kunatishia maslahi ya Amerika ... Mwelekeo mpya wa Amerika kwake umekuwa kipaumbele. Taarifa za maafisa wa Amerika zinathibitisha kile tulichokitaja hapo awali juu ya hotuba ya Biden ya tarehe 8 Julai 2021, ambapo Biden alisema, "Na tunahitaji pia kuzingatia kuongeza nguvu za kimsingi za Amerika ili kukidhi ushindani wa kimkakati na China na mataifa mengine ambazo kihakika ndizo zitakazo amua – kuamua mustakbali wetu."

Pili: Hasara zilizopatikana na Amerika nchini Afghanistan wakati wa uvamizi wake wa Afghanistan. Kama tulivyotaja hapo juu, ripoti ya BBC ya tarehe 29 Februari 2020 iliongeza, "Zaidi ya wanajeshi 2,400 wa Amerika wameuawa wakati wa mzozo."

**Yote hii yanaashira kwamba Amerika ilikuwa inaondoka Afghanistan huku ikikunja mkia wake katikati ya miguu yake, bila ya kuondoka kupitia mazungumzo ambayo yanaipa ushawishi ambao haingeweza kuupata kupitia vita!**

d- Tunatambua kuwa kuna ndugu wakweli na wenye ikhlasi ndani ya Taliban, kwa hivyo ni kwao ndio tunajielekeza sasa:

- Kwamba wasahihishe mambo kupitia kumaliza mazungumzo haya, ili wasiiwezeshe Amerika kufikia kile ambacho haingeweza kukifikia kupitia vita ...

- Na kwamba wawe na yakini kuwa suala kuu kwa Waislamu ni kurudishwa kwa Khilafah baada ya kutoweka kwa muda mrefu, kwani ni Faradhi iliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu (swt) na ni utiifu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) ...

- Na kwamba wajue kuwa kushiriki katika utawala wa mchanganyiko wa Uislamu na usekula haukubaliki kwa Mwenyezi Mungu (swt), kwa kuwa Mwenyezi-Mungu na Mwenye nguvu Muweza wa yote hakubali chochote isipokuwa kilicho kizuri …

Hii ndio haki kwani Mwenyezi Mungu (swt) asema,

[فَمَاذَا بَعْدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ]

**“Na kipo kitu gani baada ya haki, isipokuwa upotovu tu?”** [TMQ Surah Yunus 10:32].

Na kufuata Haki pekee ndiko kutakakoiokoa Taliban, nchi, watu wake na Waislamu wote ... Hivi ndivyo Hizb ut Tahrir anavyokushaurini sasa, kama vile tulivyokushaurini mwanzoni mwa utawala wenu kutangaza Khilafah. Lakini, mlikataa na kisha mkajua kuwa mumekosea kwa kukataa huko, kama ilivyosemwa na Mullah Omar, Mwenyezi Mungu (swt) amrehemu, katika moja ya vikao vyake, lakini wakati huo ilikuwa ishachelewa ... Na sisi hapa tena tunarudia ushauri ule ule, hivyo basi je sasa kuna majibu chanya?

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ]

**“Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa.”** [TMQ Surah Al-Anfal 8:24]

**09 Dhul Hijjah 1442 H**

**19 Julai 2021 M**



Email: info@uqab.or.ke






Email: info@uqab.or.ke